**HOTUBA YA NAIBU WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MH. DKT. DOTTO BITEKO (MB), KATIKA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI - ARUSHA, 28 APRILI 2024**

Mhe. Deogratius Ndejembi, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu);

Mhe. Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu);

Mhe. Patrobas Paschal Katambi (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu),

Mhe. Ummy Nderiananga, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu);

Mhe. Marry Ngelela Maganga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu),

Mhe. Paul Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Arusha,

Ndugu Missaile Albano Musa, Katibu Tawala Mkoa wa Arusha;

Mheshimiwa Felician Gasper Mtahengerwa, Mkuu wa Wilaya ya Arusha;

Bi. Khadija Mwenda, Mtendaji Mkuu Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA),

Bi. Suzanne Ndomba-Doran, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE),

Ndugu Tumain Nyamhokya, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),

Ndugu Henry Mkunda, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),

Ndugu Caroline Khamati Mugalla, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa Nchi za Tanzania, Burundi, Kenya, Rwanda and Uganda,

Viongozi na Wafanyakazi wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi Zake,

Ndgu Wandishi wa Habari

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.......**

Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani, kwa lengo la kuhamasisha waajiri, wafanyakazi na umma kwa ujumla kuweka mikakati ya kupunguza kama sio kuzuia kabisa magonjwa na ajali zinazotokea kazini.

Awali ya yote napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuwaletea maendeleo Watanzania. Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake tumeshuhudia mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Pia Mheshimiwa Rais yuko mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa Usalama na Afya wa wafanyakazi unaimarishwa katika nchi yetu. Kama mnavyokumbuka katika sherehe za mei mosi zilizofanyiaka mwaka jana, pale Morogoro, aliahidi kuimarisha tasnia ya usalama na afya mahali pa kazi katika Nchi yetu

kwa kuridhia mikataba miwili ya afya na usalama na afya mahali pa kazi pamoja na kuimarisha Taasisi yetu ya OSHA inayosimamia masuala ya usalama na afya mahali pa kazi. Ahadi hizo amezitekeleza. Mchakato wa kuridhia mikataba hiyo uko katika hatua nzuri na hivi karibuni tutaipeleka Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa ili utekelezaji wake uanze mara moja. Sambamba na hilo, Mheshimiwa Rais ametoa vitendea kazi kwa Taasisi ya OSHA kama alivyoahidi ili kuongeza uwezo wa Taasisi hiyo kutekeleza majukumu ya kusimamia usalama na afya kwa Wafanyakazi. Mheshimiwa Rais, amekuwa mstari mbele kuhakikisha kuwa Nguvu Kazi ya Taifa inalindwa na ataendelea kuiimarisha Taasisi ya OSHA ili iweze kusimamia kwa karibu utekelezaji wa **Sheria Na. 5 ya Afya na Usalama mahala pa kazi ya mwaka 2003**, lengo ni kuhakikisha kwamba maeneo yote ya Kazi Nchini yanakuwa na mifumo madhubuti ya kuwakinga wafanyakazi dhidi ya ajali na magonjwa yatakanayo na kazi.

Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendela kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutimiza majukumu yake ya kuwaletea maendeleo Watanzania.

Nitumie fursa hii kumpongeza pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anazofanya kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu.

Ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutuongoza vema katika Ofisi yetu na kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge latu Tukufu. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Waziri wote, Makatibu Wakuu wote na Viongozi mbalimbali walioko katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano wanaotoa katika kutekeleza majukumu na wajibu tulionao katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Uongozi wa Mkoa wa Arusha hususan Mkuu wa Mkoa, Mhe. **Paul Makonda**, kwa kukubali kuwa mwenyeji wetu katika maadhimisho ya siku hii. Kwa kweli ametupatia ushirikiano wa hali ya juu lakini pia kwa mapokezi mazuri ambayo nimeyapata toka nilivyofika Mkoani Arusha.

Pia ninawapongeza Viongozi wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Shirika la Kazi Duniani (ILO) na Wadau wengine ambao kwa namna moja ama nyingine wamefanya kazi kubwa na kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha kuwa siku hii ya leo inafanikiwa. **Hongereni sana**

Kipekee nitoe pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho haya chini ya uongozi wa Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi. Khadija Mwenda kwa kunipa heshima ya kuwa Mgeni Rasmi katika siku hii muhimu ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani.

Nitoa pia pongezi kwa wadau wa Masuala ya Usalama na Afya mahali

pa kazi, ambao wamekuja kwenye maonesho na kutoa huduma mbalimbali kwenye maadhimisho haya katika viwanja hivi vya General Tire, Arusha. **Asanteni sana.**

Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wananchi wote wa Mkoa wa Arusha hasa Wafanyakazi kwa kujitokeza kwa wingi katika siku hii muhimu ambapo Tanzania inaungana na Mataifa mengine kuadhimisha siku ya Usalama na Afya mahali pa Kazi Duniani.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Nimepewa taarifa kwamba, kuelekea Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Usalama Mahala pa Kazi Duniani, kwa mwaka 2024, kumekuwa na shughuli mbalimbali ambazo zimeratibiwa na OSHA kwa kushirikiana na wadu wengine. Shughuli hizo ni pamoja na kutoa semina kuhusu masuala ya **Usalama na Afya Mahali pa Kazi** kwa Wahariri wa Vyombo vya Habari nchini; Mafunzo ya Usalama na Afya mahali pa kazi kwa Wafanyakazi wa Makampuni ya Uchimbaji Makaa ya Mawe wa Wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma; mafunzo kwa wajasiriamali wadogo katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Kilimanjaro, Manyara na Arusha; mafuzo ya usalama kwa Mama Lishe pamoja na kuwapatia majiko bora yanayotumia nishati safi ya gesi; na mafuzo kwa waendesha badaboda wa mkoa wa Arusha. Niwapongeze sana OSHA na Wadau wote walioshiriki katika kutekeleza jukumu hili kwa ustawi wa Wafanyakazi na Umma kwa ujumla. Nitoe wito kwamba zoezi hili liwe endelevu na lifanyike Nchi nzima kadri uwezo utakavyo ruhusu.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Leo hii tuko hapa katika kuadhimisha siku ya Usalama na Afya mahali pa Kazi Duniani. Kama mnavyokumbuka, chimbuko la siku hii ilikuwa ni harakati za Chama cha Wafanyakazi Duniani katika kuwakumbuka wafanyakazi waliopoteza maisha, kupata ulemavu ama kupata magonjwa yatokanayo na kazi wakiwa wanatekeleza majukumu yao. Mtakumbuka pia kuwa siklu hii ilianzia kuadhimishwa huko New York, Marekani mwaka wa 1996.

Hata hivyo, ni jambo la faraja kuona kwamba Shirika la Kazi Duniani (ILO) liliamua kuunga mkono Chama cha Wafanyakazi Duniani na kubadilisha maudhui ya siku hii ambapo badala ya kukusanyika na kuwasha mishumaa ya maombolezo kwa wafanyakazi waliopoteza maisha wakiwa kazini, ILO waliona ni vema kuibadilisha siku hii ili iwe siku ya kutafakari, kuhamasisha na kuweka mikakati ya kuendelea kuboresha mazingira ya kazi ili kuwalinda wafanyakazi dhidi ya vihatarishi vya ajali, magonjwa na vifo mahali pa kazi. Hivyo basi, kuanzia mwaka 2003 zaidi ya Nchi 110 Duniani kote huadhimisha siku hii kwa lengo la kuwahamasisha wadau kuendelea kuzingatia kanuni bora za usalama na afya kazini na kujenga uwezo wa Nchi hizo katika kuweka Sera na Mikakati ya kuzuia ajali na magonjwa kazini.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Kama mnavyofahamu huu ni mwaka wa ishirini (20) tangu tulipoanza kuadhimisha siku hii hapa Nchini kwetu kuanzia mwaka 2004. Kila mwaka Shirika la Kazi Duniani, ILO limekuwa likitoa kauli mbiu mbalimbali kulingana na wakati na matukio yanayokuwepo duniani katika mwaka husika na kauli mbiu hizo zimekua zinalenga kuhamasisha

Waajiri na Wafanyakazi kufanya juhudi za makusudi ili kuzuia magonjwa na ajali kazini. Na mwaka huu kauli mbiu ni: ***"Athari za mabadiliko ya tabia nchi katika usalama na afya kazini (The impacts of climate change on occupational safety and health)".*** Hapa kwetu Tanzania, kauli mbiu hii inaenda sambamba na kampeni ya kusajili maeneo ya kazi katika harakati za kupunguza hizo athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Kama mnavyojua, Kauli Mbiu hii inaisisitiza kuhusu uhifadhi wa mazingira ili kuepuka athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Wataalamu wetu wa masuala ya mazingira wanatuambia kwamba kuna vyanzo vikuu viwili vya mabadiliko ya tabianchi ambavyo ni vyanzo vya kiasili na vyanzo vinavyotokana na shughuli za kibinadamu. Vyanzo vya asili ni ni kama vile; miale ya jua, mchepuko wa sayari ya Dunia katika mzunguko wake, mtengenezezeko wa milima na mwelekeo wa mabara, utokaji wa asili wa gesi za hewa ukaa zinazoleta mrundikano wa gesi joto katika angahewa na ongezeko la joto duniani.

Vyanzo vinavyotokana na shughuli za kibinadamu ni kama vile: uvamizi na uvunaji wa misitu usio endelevu kwa ajili ya mbao, mkaa, shughuli za kilimo, makazi, na ufugaji; uchomaji moto misitu na mbuga kwa ajili ya kurina asali na uwindaji wa wanyama wadogo; ongezeko la viwanda duniani ambavyo mifumo yake ya uzalishaji hutoa hewa ukaa na kemikali zenye madhara katika tabaka la ozoni; matumizi ya mbolea za viwandani katika kilimo; uchimbaji wa madini unaotumia mitambo na kemikali zenye athari za kimazingira kama vile makaa ya mawe, urani na mafuta.

Ushahidi na viashiria vya kuthibitisha kuwepo kwa mabadiliko ya tabianchi ni kama vile kuwepo na mabadiliko ya vipindi vya mvua mara kwa mara; kukauka kwa vyanzo vya maji; ongezeko la joto duniani; kutoweka kwa baadhi wadudu, mimea, na wanyama wa asili; kutotabirika kwa majira ya mwaka (vuli, masika, kiangazi na kipupwe).

Baadhi ya madhara au athari zilizotokana na mabadiliko ya tabianchi katika sehemu mbalimbali za nchi yetu ni kama vile:

- Ongezeko la joto linaloleta athari za aina mbalimbali. Kwa mujibu wa machapisha katika majirida mbalimbali, inaonesha kuwa wastani wa joto umekuwa ukiongezeka mfululizo katika Nchi yetu kati ya 0.1°C hadi 0.5°C kwa miaka kumi tangu 1981. Wastani wa joto unaweza kutarajiwa kuongezeka kati ya 2.3°C na 5.2°C mwishoni mwa karne ya 21.
- Uhaba wa maji unaotokana na kukauka kwa vyanzo mbalimbali vya maji, hali inayoathiri uzalishaji wa umeme na shughuli nyine za kiuchumi.
- Uharibifu wa miundombinu unaotokana na upepo mkali, mvua kubwa na mafuriko.
- Ongezeko la magonjwa kwa baadhi ya sehemu za Nchi yetu mfano malaria, zika dengi, kichocho, nk
- Migogoro ya ardhi miongoni mwa jamii zetu hasa wakulima na wafugaji ambao mifumo yao ya uzalishaji imeathiriwa na upungufu wa ardhi yenye rutuba, malisho ya mifugo na maji.
- Upungufu wa uzalishaji wa chakula unaotokana na mabadiliko ya misimu ambayo hupelekea hali ya ukame au mvua kubwa ambavyo huharibu mazao.

Kwa upande mwinigne, katika Ulimwengu wa Kazi mabadliko ya tabianchi yamesababisha ongezeko la vihatarishi sehemu za kazi. Vihatarishi hivyo mara nyingi vinaweza kusababisha ajali na magonjwa kama vile saratani, ugonjwa wa moyo na mishipa, mfumo wa kupumua, kuzorota kwa mifupa na misuli na shida za afya ya akili. Wafanyakazi wanoathrika zaidi ni wale wanaofanyakazi za wazi (ujenzi, kilimo, na usafirishaji), wafanyakazi wanofanya kazi katika mazingira ya joto, akinamama wajawazito, waafanyakaazi wenye ulemavu, pamoja na wajasilai mali wadogo

Matokeo ya madaliko ya tabianchi husababisha kuongezeka kwa joto sehemu za kazi. Kwa mujibu wa ripoti ya shirika la kazi dunioani takribani wafanyakazi 22.85 milioni wanapata ajali na 18,970 wanafariki duniani kote kutokana na madhara ya ongezeko la joto mahali pa kazi. Mabadiliko ya tabianchi pia yamesababisha kuongezeka kwa mionzi ya jua amabayo inasababisha salatani ya Ngozi. Ongezeko na mionzi ya jua inagharimu takribani maisha ya watu 18,960 kila mwaka.

Athari nyingine za mabadiliko ya tabianchi katika sehemu za kazi ni kuchafuka kwa hewa safi mahali pa kazi na hali hii inasabaabisha magonjwa kama sarani ya mapafu, magonjwa ya mfumo wa hewa, damu na macho. Kwa mujibu wa Shirika la Kazi Duniani, ILO inaonesha kuwa takribani wafanyakazi 860,000 wanapotezamaisha kutokana na hali hiyo.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Pamoja na kwamba suala la mabadiliko ya tabianchi ni janga la Dunia nzima, katika Nchi yetu upo uwezekano wa kupambana au kuhimili tatizo hili kwa mipango na mikakati inayoendelea kutekelezwa maeneo mbalimbai Nchini. Baadhi ya mipango na mikakaati inayotekelezwa na ambayo inatakiwa kuwa endelevu ili kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi ni kamaa vile:

- Kutunza mazingira kama vile kupanda miti, kutunza misitu na rasilimali zake, vyanzo vya maji, kuacha kulima au kuchunga mifugo kwenye vyanzo vya maji. Katika mkakati huu Nchi yetu tumewka lengo la kupanda miti takribani Milioni 276 kila mwaka ambayo ni wastani wa miti milioni 1.5 kwa kila Halmashauri.
- Kupunguza matumizi ya mbolea hasa ya chumvichumvi na kuwekeza katika mbolea za asili na kupumzisha mashamba, pamoja na kufanya kilimo mseto; kilimo cha mazao mchanganyiko kwa lengo la kutunza rutuba na kuhifadhi mazingira. Hii itaepusha matumizi ya pembejeo za kisasa ambazo zina madhara kwenye ardhi na viumbe hai wanaopatikana ardhini na kwenye mimea mingine pamoja na athari za kibinadamu zinatotokana na vyakula vinayopatikana.
- Kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua ili kukabilia na athari za upungufu wa maji hasa wakati wa ukame.
- Kuzingatia matumizi endelevu ya maliasili, misitu, ardhi, maji hususan katika maeneo ambayo shughuli za kibinadamu hazitakiwi kufanyika.
- Kuepuka kuishi au kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo hatarishi kama vile maeneo ya mabondeni au maeneo yenye miamba ambayo yanaaririka kirahisi na mabadiliko ya tabia Nchi hussan kipindi cha mvua kubwa na upepo mkali.

- Kufuata maelekezo ya wataalamu wa masuala ya mazingira, kilimo na ufugaji.
- Matumizi ya nishati mbadala kama vile gesi na nishati ya jua ili kupunguza utekemezi wa mkaa na kuni hali ambayo itasidia kulinda misitu yetu.
- Kuhamasisha, kuheshimu na kutambua kuwa Mazingira salama na yenye afya kazini ni kanuni na haki ya msingi mahali pa kazi na pia kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi zina madhara katika usalama afya za wagfanyakazi wakiwa kazini. Na hivyo ni vema kuweka juhudi za kuzipunguza.

Kwa maana hiyo ningependa kuchukua fursa hii kuwataka Waajiri wote wakishirikiana na Wafanyakazi na Jamii inayowazunguka, kuhakikisha kuwa juhudi za makusudi zinafanyika ili kulinda mazingira na hatimae tuweze kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Moja ya majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kulinda Usalama na Afya wa Wafanyakazi wanapokua maeneo ya kazi. Usalama na Afya mahali pa kazi ni moja kati ya masuala ya kazi kama ilivyo masuala mengine ya wafanyakazi.

Ikiwa suala la usalama na afya mahali pa kazi halitazingatiwa kuna athari nyingi ikiwa pamoja na upotevu wa maisha ya wafanyakazi na pia kuathiri utendaji wa kazi wakati wafanyakazi waliomia wakiendelea kupata matibabu. Kwa maana hiyo ningependa kuchukua fursa hii kuwataka Waajiri wote Nchini wachukue hatua ya kuhakikisha kwamba wanalinda

usalama na afya za wafanyakazi wao kama yalivyo matakwa ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi Namba 5 ya mwaka 2003.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Upo ukweli kwamba magojwa, ajali na vifo vinavyotokea sehemu za kazi vinaweza kuzuilika kwani dalili za kutokea kwake zinaanza kuonekana mapema. Ili kuzuia magonjwa, ajali na vifo inatakiwa kuweka mifumo sahihi ya usalama na afya mahali pa kazi na kuzingatia sheria na kanuni za Usalama na Afya sehemu za kazi.

Mifumo hiyo inatakiwa kuzingatia vihatarishi vya dharura na utayari wa kukabiliana na hali ya dharura kama vile ilivyotokea wakati wa UVIKO-19. Kwa bahati mbaya waajiri wengi hawajaweka hiyo mifumo na wengine hawana ufahamu wa namna ya kuweka mifumo hiyo, hivyo nawasisitiza na kuwaomba Waajiri wote washirikiane na OSHA ili kuhakikisha mifumo hiyo inawekwa maeneo ya kazi.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Sekta isiyo rasmi na sehemu ndogondogo za kazi zina mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu. Lakini kwa bahati mbaya wafanyakazi katika sekta hii wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Mara nyingi huduma ya ukaguzi wa afya na usalama kazini haiwafikii wafanyakazi katika sekta hii. Katika sekta hii viwango vya ajali na magojwa yatokanayo na kazi yawezekana vikawa vikubwa sana. Kwa bahati mbaya kwa sasa hakuna mfumo ulioandaliwa wa kuripoti ajali na magonjwa hayo unaofanya kazi kwa sasa katika sekta hii. Hali hiyo inasababisha kushidwa kufahamu kwa uhakika hali halisi ya usalama na

afya katika sekta hiyo. Hivyo wakati tunaadhimisha Siku ya Afya na Usalama Mahala Pa kazi niwasisitize OSHA kwa kushirikiana WCF pamoja na wadau wengine kuangalia uwezekano wa kufahamu hali halisi katika sekta hii ili tuangalie namna ya kuwasaidia Watanzania hawa wasiendelee kupata madhara wakiwa kazini.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Serikali yetu inathamini na kutambua juhudi za Taasisi za umma na binafsi zinazojituma katika kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wao bila kushurutishwa. Serikali kwa kupitia Wakala wa Usalama na Afya mahali pa Kazi (OSHA), imeanzisha tuzo kwa Taasisi zinazoonyesha juhudi katika kuboresha mazingira ya kazi. Napenda, nichukue furusa hii kuzipongeza Taasisi zitakazofanikiwa kupata hizo tuzo kwa mwaka huu. Tuzo hizo zitatolewa katika hafla maalum itakayofanyika usiku wa Aprili 30 ambapo wadau mbalimbali wa masuala ya usalama na afya kazini watakabidhiwa tuzo hizo kwa kadri ilivyopangwa na nina imani kuwa kila mmoja wenu atapata Tuzo. Nichukue fursa hii kuwaasa wale watakaopata Tuzo, wasibweteke na hizo Tuzo, bali waendelee kuimarisha usalama na afya kwa wafanyakazi wao.

***Ndugu Wafanyakazi na Waajiri,***

Nikielekea Kuhitimisha Hotuba yangu, sote tunafahamu kuwa zimesalia siku tatu tu tufikie kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei Mosi 2024. Namna bora ya kuadhimisha siku ya Mei Mosi ni kwa Wafanyakazi kujitathmini kila mmoja ni kwa namna gani tumeweka juhudi za kujilinda na vihatarishi sisi wenyewe na wale tunaofanyakazi pamoja, na kwa kiasi gani tutashirikiana na Waajiri wetu katika kutengeneza

mazingara ya kudumisha haki za msingi za wafanyakazi wakiwa kazini.

Niwasihi Wafanyakazi, Waajiri na Wananchi wote wa Mkoa wa Arusha na mikoa ya jirani kujitokeza kwa wingi katika siku ya kilele cha Mei Mosi ili tuweze kusherehekea siku hii kwa pamoja. Kwa wale watakaoweza kufika katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid hapa Jijini Arusha siku ya tarehe 1 Mei,2024 karibuni sana.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Napenda nirudie kutoa pongezi zangu za dhati kwa Wafanyakazi na Wananchi wote wa mkoa wa Arusha kwa kufanikisha maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani mwaka huu, na niwakumbushe tena kauli mbiu ya mwaka ambayo ni "***Athari za mabadiliko ya tabia nchi katika usalama na afya kazini".***

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Mwisho ningependa kusisitiza kuwa, serikali yetu inayoongowa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itaendelea kusimamia suala la Usalama na Afya Mahala pa Kazi, hivyo tunawaomba wadau wetu muendelea kushirikiana na Mheshiwa Rais ili kutimiza azima hii ambayo inalenga kupunguza au hata ikiwezekana kuondoa kabisa vifo, ajali, magonjwa na madhara yatokanayo na kazi. Kwa pamoja kama Taifa tutaweza kupata suluhisho la matatizo ya usalama na afya yanayowapata wafanyakazi wakiwa kazini.

Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Serikali, kwa mara nyingine napenda kuwashukuru wote mlioshiriki kikamilifu katika maadhimisho

haya na ninawatakia siku njema.

**Asante kwa kunisikiliza.**